- ***Mhe. Joel Nanauka (Mb.), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana;***
- ***Mhe. Ali Suleiman Ameir, Waziri wa Kazi, Ajira, Vijana na Uwezeshaji, Zanzibar;***
- ***Mhe. Albert John Chalamila, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam;***
- ***Wahe. Mawaziri na Naibu Mawaziri mliopo;***
- ***Ndg. Abbas Mtemvu, Mwenyekiti wa CCM, Mkoa wa Dar es salaam;***
- ***Mhe. Hawa Chakoma (Mb.), Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii;***
- ***Mhe. Zainab Katimba (Mb.), Mwenyekiti wa Umoja wa Wabunge Vijana Tanzania;***
- ***Waheshimiwa Wabunge mliopo;***
- ***Ndg. Mohamed Ali Kawaida, Mwenyekiti wa UVCCM Taifa;***
- ***Bi. Jenifa Omolo, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana;***
- ***Bi. Salama Mbarouk Khatib, Katibu Mkuu, Wizara ya Kazi, Ajira, Vijana na Uwezeshaji, Zanzibar;***
- ***Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu mliopo;***
- ***Ndg. Abdul Rajabu Mhinte, Katibu Tawala wa Mkoa wa Dar es Salaam;***
- ***Mhe. Saad Mtambule, Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni;***
- ***Mhe. Songoro H. Mnyonge, Mstahiki Meya wa Manispaa ya Kinondoni;***
- ***Bi. Susan Ngongi Namondo, Mratibu Mkazi wa Umoja wa Mataifa nchini Tanzania;***
- ***Wawakilishi wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa na Taasisi za Kimataifa nchini;***
- ***Viongozi wa dini;***
- ***Wakuu wa Taasisi zinazoongozwa na Vijana na viongozi wa mashirika ya vijana;***
- ***Vijana wote mliopo;***
- ***Waandishi wa habari;***
- ***Mabibi na mabwana.***

Kazi na Utu...

Vijana wa Tanzania, Mambo Vipi?

Jamani, tupo hapa tupo Dar es Salaam au tupo kwenye Mkutano wa Mabosi wa Bodi ya Wakurugenzi?

Mambo Vipi? Sasa nimeamini kwamba niko kwenye mkutano wa vijana unaofanyika katika Jiji la Dar es Salaam.

Kabla sijaanza hotuba yangu, naomba kuuliza swali moja? Ni wangapi kati yenu hapa mnatamani kumiliki kampuni zenu, kuwa na maisha mazuri na kumiliki vitu vizuri?

Swali lingine kwenu. Ni wangapi kati yenu hapa mnaona kwamba ndoto zenu ni kubwa kuliko hali halisi mifukoni mwenu? Hapo najua ndipo wengi wetu tulipo.

Vijana wa Tanzania, hakuna dhambi yoyote kwa kijana kuwa na ndoto kubwa katika maisha yake.

Leo nimekuja hapa ili kuwaambia kwamba Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inajua matamanio na ndoto zenu. Inafahamu hali zenu. Imesikia kilio chenu ambacho mmekuwa mkikitoa kila fursa ilipopatikana.

Katika maadhimisho haya ya mwaka mmoja madarakani wa Awamu ya Pili ya Serikali ya Dkt. Samia Suluhu Hassan, nimekuja hapa tuzungumze ili mjue serikali imefanya nini, imepanga kufanya nini zaidi na kuwapa moyo na matumaini kwamba kesho yenu ni nzuri.

Kabla ya kusema nini ambacho serikali imefanya, ningependa kuzungumzia kuhusu takwimu muhimu ili walau sote tujua halisi iliyopo na ukubwa wa changamoto tulizonazo.

Mwaka 2012, Takwimu za Sensa ya Watu na Makazi, zilionyesha kwamba Tanzania ilikuwa na watu milioni 44.9. Sensa ya mwaka 2022 imeonyesha

kwamba idadi ya watu wenye umri chini ya miaka 35 ambao wengi wao ni vijana, imefikia watu milioni 46.9. Hii maana yake nini? Hii maana yake ni kwamba idadi ya vijana iliyopo Tanzania leo ni kubwa kuliko idadi ya Watanzania wote miaka 14 tu iliyopita. **Naomba kurudia, Tanzania leo ina vijana wengi kuliko Watanzania wote waliokuwa hai mwaka 2012**.

Takwimu ya pili. Kila mwaka, Watanzania 850,000 wanahamia mijini. Takwimu hii maana yake ni kwamba kunakuwa na jiji jipya walau kila mwaka. Lakini huko mjini kwenye ajira kukoje? Kwa mujibu wa Taarifa ya Uchumi wa Nchi ya mwaka 2024, Idadi ya vijana wanaoingia katika soko la ajira ni 900,000 lakini wanaokadiriwa kupata ajira rasmi ni takribani watu 90,000. Hii maana yake ni kijana mmoja katika kumi wanaoingia sokoni ndiyo hupata ajira.

Ukiziangalia takwimu hizi, picha unayopata ni changamoto kubwa ya ajira kwa vijana, makazi, afya, maji, nishati, usalama, umuhimu wa biashara bunifu, upatikanaji wa mikopo, umuhimu wa sekta binafsi na sekta isiyo rasmi na uchumi jumuishi.

MASUALA YA VIJANA KUHAMIA OFISI YA RAIS

Jambo kubwa la kwanza ambalo Rais Samia amelifanya kwa vijana ni kitendo cha kuhamisha masuala ya vijana kuwa chini ya Ofisi ya Rais. Hii ni kwa sababu masuala ya vijana ni mtambuka. Masuala ya ajira yanahusu Wizara ya Kazi, masuala ya kilimo kwa vijana yanagusa Wizara ya Kilimo, masuala ya biashara bunifu yanagusa Wizara ya Viwanda na Biashara, masuala ya elimu yanagusa Wizara ya Elimu.

Hatua ya Mhe.Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kuweka mambo ya vijana chini ya ofisi yake kumeonyesha namna anavyotambua ukubwa wa jambo hili na ukubwa wa utatuzi. Kwa changamoto ilivyo, wizara moja au taasisi moja peke yake isingeweza.

Kuwa chini ya Rais kunarahisisha uratibu lakini pia kuonyesha jambo linaangaliwa katika ngazi ya juu kabisa.

Uamuzi huu umempa mheshimiwa Rais uwezo wa kufuatilia kwa karibu namna sera, mipango, fedha na uwekezaji wa Serikali vinavyowafikia vijana na kuboresha maisha yao.

MIKOPO YA SHILINGI BILIONI 200 KWA VIJANA

Ndugu Washiriki, Serikali, chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imetenga Shilingi bilioni 200 kwa ajili ya kuwawezesha vijana kiuchumi. Programu hii inahitaji usimamizi wa pamoja wa Serikali na taasisi zinazotekeleza.

Kwa mantiki hiyo, ninaziagiza Wizara za kisekta kufanya uwezeshaji kulingana na mahitaji ya uzalishaji, na kufuatilia matumizi ya mitaji pamoja na maendeleo ya shughuli zinazofadhiliwa.

Muhimu ni kuhakikisha vijana, wanawake na wenye ulemavu hasa walioko vijijini wanafikiwa kwa kuzingatia mazingira yao.

Muhimu zaidi fedha hizo zinapaswa kuhakikisha kuzaliwa kwa biashara mpya, fursa mpya kujitokeza, wajasiriamali wapya kusaidiwa na biashara zilizoanza kukua.

Mambo matatu ni muhimu wahusika wakayawekea mkazo ili hatua hii kubwa ya Mheshimiwa Rais izae matunda.

La kwanza; ni kueleweka kwa vigezo na masharti na urahisi wa kufikiwa na vijana. **La pili**; ni uwepo wa uwazi na haki kwenye kutolewa kwake. Kwamba ni ijulikane waliopata wamepataje, ni akina nani na utaratibu gani ulitumika na mwisho kuwepo na ufuatiliaji unaoonyesha matokeo ya fedha zilizotolewa.

Kupitia mkutano huo, natoa maelekezo kwamba ni marufuku kwa fedha hizi za uwezeshaji kutolewa kwa kujuana na kufahamiana. Kutolewa kwa kubagua

vijana wa mijini na vijijini, wanawake na wanaume au kuwaweka kando vijana wenye ulemavu.

Ndoto na uchungu wa maisha wa kijana wa Kigoma ni sawa na ile ya kijana wa Dar es Salaam. Ndoto ya kijana wa Arusha ni sawa na ndoto wa kijana wa Mtwara. Ndoto wa kijana wa Dodoma haina tofauti na ndoto ya kijana wa Mbeya.

UCHUMI UNAOWAPA VIJANA NGUVU YA KUFANIKIWA

Ndugu vijana, tunapozungumza kuhusu maendeleo ya nchi yetu, tunazungumza kuhusu barabara, reli, bandari, nishati na miradi mikubwa ya kimkakati. Hayo ni mambo muhimu sana. Lakini leo nataka tuyaangalie kwa macho ya kijana wa kawaida.

Kuna miradi mingi mikubwa ambayo Mhe.Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ameizindua baada ya kukamilika au kutangaza kuanza kwa ujenzi ambayo itakuwa na manufaa makubwa kwa vijana katika kutatua changamoto nilizozitaja.

Mathalani, tunapozungumza kuhusu Mradi wa Umeme wa Bwawa la Julius Nyerere wenye uwezo wa kuzalisha megawati 2,115, hatuzungumzii umeme peke yake. Tunazungumzia kijana anayeweza kufungua karakana ya kisasa. Tunazungumzia kijana anayeweza kuanzisha kiwanda kidogo cha kusindika mazao.Tunazungumzia kijana anayefanya kazi za kidijitali kutoka kijijini kwake.

Tunapozungumza kuhusu reli ya kisasa ya SGR, hatuzungumzii treni peke yake. Tunazungumzia fursa za usafirishaji, biashara, maghala, utalii, huduma na ajira.

Tunapozungumza kuhusu uwekezaji katika bandari, madini, kilimo na viwanda, tunazungumzia uchumi ambao unapaswa kufungua milango kwa vijana wengi zaidi.

Changamoto ambayo sasa inaendelea kufanyiwa kazi ni kuhakikisha tunajenga uwezo wa vijana kutumia miundombinu hiyo kujipatia kipato. Hatupendi kuona miradi mikubwa inajengwa, halafu vijana wa maeneo yanayozunguka miradi hiyo wanabaki watazamaji.

Tunataka wawe mafundi, wahandisi, watoa huduma, wazalishaji, wafanyabiashara na hatimaye wamiliki wa biashara zinazokua kutokana na uwekezaji huo.

Kwa maelezo hayo, ninazitaka wizara na taasisi zinazotekeleza miradi mikubwa ya serikali kuweka mkazo katika kuunganisha miradi hiyo na fursa halisi za vijana.

Tusiishie kutangaza thamani ya mradi. Tuonyeshe pia vijana wangapi wamepata ujuzi, wangapi wamepata kazi, wangapi wameanzisha biashara na wangapi wameongeza kipato chao kutokana na mradi huo. Huo ndiyo utakuwa ushahidi wa maendeleo yanayogusa maisha ya wananchi.

DIRA 2050 NA MANUFAA KWA VIJANA

Ndugu Washiriki,

Serikali ya Rais Samia imeegemeza mipango yake ya muda mfupi, wa kati na mrefu kupitia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050. Lengo la Serikali ni kutaka kujenga uchumi mkubwa zaidi, wenye uzalishaji wa juu, teknolojia ya kisasa na ajira zenye staha.

Lakini nataka tujiulize swali moja. Ni nani atakayeijenga Tanzania hiyo? Jibu ni ninyi vijana ambao mko hapa sasa na wengine walioko maeneo tofauti ya Tanzania. Ukitaka kupata picha nzuri, lifikirie jambo hili kwa upeo wa kuwa kijana mwenye miaka 20 leo, mwaka 2050 atakuwa na miaka 44.

Kijana mwenye miaka 25 leo atakuwa na miaka 49. Hawa ndio watakaokuwa wahandisi wakuu, wakurugenzi wa kampuni, wakulima wakubwa, wanasayansi, wabunifu, wafanyabiashara na viongozi wa Taifa letu.

Kwa hiyo, tunapozungumzia Dira 2050, hatuzungumzii ndoto ya Serikali pekee. Tunazungumzia maisha ya vijana waliopo hapa leo. Na ndiyo maana tunapaswa kuwekeza katika elimu yao, afya yao, ujuzi wao na uwezo wao wa kuzalisha mali.

Lakini pia nataka kusema jambo muhimu.Mwaka 2050 ni dira yetu. Lakini maisha ya vijana yanaendelea leo kwa sababu wanahitaji ajira leo, wanahitaji mitaji leo, wanahitaji huduma bora leo. Kwetu sisi Viongozi kwenye utekelezaji wa Dira

wajibu wetu ni kupambana kuhakikisha kuwa mafanikio ya Dira 2050 lazima yaanze kuonekana katika hatua tunazochukua kila mwaka.

ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

Ndugu Washiriki, katika mwaka wa masomo 2026/27, hadi tarehe 21 Oktoba, Serikali imepanga mikopo na ruzuku zenye thamani ya Shilingi bilioni 820.4 kwa wanafunzi 256,010 katika awamu mbili. Sambamba na uwekezaji huo katika elimu ya juu, Serikali inaendelea kupanua mafunzo ya ufundi stadi kupitia ujenzi wa vyuo katika maeneo mbalimbali nchini. Kupitia uwekezaji huu, vijana wengi zaidi wanapata elimu na ujuzi unaowawezesha kuajiriwa, kujiajiri na kuendesha shughuli za uzalishaji. Ninazielekeza taasisi za elimu na mafunzo kuimarisha ushirikiano na waajiri na sekta binafsi katika kuandaa mitaala na kutoa mafunzo kwa vitendo, ili vijana wahitimu wakiwa na uwezo wa kutumia teknolojia na kutekeleza kazi zinazohitajika katika uchumi wetu.

UKUZAJI UJUZI NA AJIRA KWA VIJANA

Katika kukuza ujuzi na maandalizi ya vijana kuingia katika soko la ajira, Serikali inaendelea kuimarisha programu za uanagenzi na mafunzo kwa vitendo katika sekta ya umma na binafsi. Katika kutekeleza suala hili, tarehe 28 Septemba mwaka huu nilipofungua kikao cha Wenyeviti wa Bodi na Wakuu wa Taasisi, Jijini Arusha, nilitoa maelekezo, ya kutoa nafasi za mafunzo kwa vitendo kwa wahitimu wasiopungua 10,000 katika mashirika ya umma, na vijana wengine wasiopungua 20,000 kupitia sekta binafsi. Nafahamu kwamba suala hili linafanyiwa kazi kwa kina na wahusika na muda si mrefu Watanzania wataambiwa tumefikia wapi.

FURSA ZA AFCON 2027

Ndugu Washiriki, mwakani Tanzania, Kenya na Uganda zitakuwa wenyeji wa mashindano ya AFCON. Jambo hili lisingewezekana kama Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan asingekubali sisi tuwanie kuwa wenyeji na kufanya uwekezaji

ambao umeifanya Tanzania kuonekana nchi iliyojiandaa zaidi miongoni mwa waandaaji.

Mmesikia CAF wameamua kwamba Tanzania ipewe maeneo matatu ambako AFCON itachezwa – Dar es Salaam, Arusha na Zanzibar. Uganda wamepewa miji miwili na Kenya mji mmoja tu. Hii ni heshima kubwa kwetu.

Hata hivyo, AFCON haitakiwi kuishia kwenye ujenzi wa viwanja vizuri vya mpira, ujio wa wageni wengi na ujenzi wa hoteli. Ni muhimu tukaenda mbali zaidi kwa kuona kwamba hii ni fursa ya ajira kwa vijana, ongezeko la vipato na ongezeko la stadi za maisha za kudumu.

Kupitia mkutano huu, naagiza Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania (TFF), kukaa chini na Chuo cha VETA na pengine vyuo vya kati nchini kuangalia uwezekano wa kutoa mafunzo mafupi kwa vijana wa Kitanzania ili wapate fursa ya kutoa huduma kwa wageni watakaokuja.

Ziko takwimu zinaonyesha kwamba maelfu ya vijana wa Morocco na Ivory Coast walipewa mafunzo ya lugha za kigeni, ukarimu, utembezaji watalii, mapokezi, ulinzi wa viwanja nk.

Hata kama wahusika hawatapata malipo makubwa au kazi za kudumu, watakuwa wamepata ujuzi wa kudumu utakaowasaidia kwenye maisha yao ya baadaye.

Naamini kabisa TFF wakiwasiliana na CAF na wenzao wa Morocco na Ivory wanaweza kujua ukubwa wa mahitaji na sisi serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi tunaweza kutumia vyuo vyetu kuandaa mafunzo ya muda mfupi ili fursa za AFCON2027 zisitutupe. Hapo mnaonaje?

MSISITIZO KATIKA KUENDELEZA AJENDA YA VIJANA

Ndugu Washiriki, ili kulinda mafanikio yaliyopatikana na kuendelea kusukuma ajenda ya maendeleo ya vijana ni lazima mipango yetu iwaandae vijana kushiriki katika uchumi wenye ushindani, kutumia teknolojia mbalimbali zinazoibukia na kuongeza uzalishaji. Hivyo, ili kufikia lengo kuu la Ilani ya Uchaguzi ya CCM

(2025 – 2030) la kukuza uchumi na kuimarisha ustawi wa wananchi, ningependa kusisitiza masuala muhimu yafuatayo:-

Kwanza, ni kujumuisha maendeleo ya vijana katika mipango na bajeti zetu. Wizara, taasisi za umma na mamlaka za Serikali za Mitaa zijumuishe masuala ya maendeleo ya vijana katika mipango na bajeti zao. Kila taasisi ibainishe shughuli itakazotekeleza, vijana inaolenga kuwafikia na matokeo yanayotarajiwa. Ofisi ya Rais – Maendeleo ya Vijana isimamie uratibu wa utekelezaji kupitia Mfumo wa Uratibu wa Kitaifa wa Masuala ya Maendeleo ya Vijana tuliozindua leo.

Pili, kuandaa vijana kwa ajira na uzalishaji. Taasisi zenye dhamana ya elimu, mafunzo na ajira kushirikiana na waajiri kuhakikisha vijana wanapata ujuzi unaohitajika katika shughuli za uzalishaji na huduma. Ushirikiano huo uongeze nafasi za tarajali, uanagenzi na urasimishaji wa ujuzi, pamoja na kuwawezesha vijana kutumia teknolojia katika kazi zao. Vijana walio nje ya mfumo rasmi wa elimu wafikiwe pia, kulingana na mahitaji na shughuli wanazozifanya.

Tatu, kuwezesha ukuaji wa biashara za vijana na ajira. Ninazitaka taasisi zinazotoa huduma za uwezeshaji kuwaunganisha vijana na mitaji, maeneo ya uzalishaji, vifaa, utaalamu na masoko. Usimamizi na ufuatiliaji usiangalie zaidi kiasi cha mikopo iliyotolewa, bali uoneshe biashara zilizoanzishwa, zinazokua na ajira zinazozalishwa. Taasisi za umma pia zinawajibika kuchangia kwa kutoa

fursa za ununuzi wa bidhaa na huduma za vijana na kulipa kwa wakati kwa mujibu wa mikataba.

Nne, kuendeleza bunifu na matumizi ya teknolojia. Taasisi za utafiti, elimu, teknolojia na uwezeshaji zishirikiane na sekta binafsi kusaidia bunifu za vijana kufikia hatua ya matumizi na uzalishaji wa kibiashara. Wabunifu wapate huduma za kujaribu bidhaa, kulinda bunifu zao na kufikia wawekezaji na masoko. Kipaumbele kiwekwe pia katika suluhisho zinazoongeza tija na kushughulikia mahitaji ya wananchi katika uchumi wa kidijitali na uchumi wa kijani.

UJUMBE WANGU KWA VIJANA WA TANZANIA

Ndugu zangu vijana,

Ninapokaribia kuhitimisha hotuba yangu, nataka nizungumze nanyi moja kwa moja. Ninajua kwamba si kila kijana anayenisikiliza hapa leo ana kazi. Si kila kijana ana biashara. Si kila kijana ana mtaji. Na si kila kijana ana uhakika wa maisha yake ya kesho.

Lakini nataka niwaambie jambo moja.

Hali uliyonayo leo si lazima iwe mwisho wa hadithi ya maisha yako. Usikubali changamoto za sasa zikuondolee uwezo wa kuota ndoto kubwa. Endelea kujifunza. Endelea kutafuta maarifa. Endelea kubuni. Endelea kufanya kazi kwa uaminifu. Usiache kumuamini na kumuomba Mungu wako. Na endelea kuitumia kila fursa inayojitokeza kuboresha maisha yako.

Na mimi nikiwa kama kaka yenu, nina ujumbe wenu mahususi. Mama yuko jikoni anawaandalia mambo mazuri zaidi. Sisi wengine ndiyo anatutuma kumpelekea maji, kufuata chumvi dukani na vikorombwezo vingine ili msosi uwe wa maana. Sasa tusimsumbue bila sababu kwani tutaharibu msosi. Tusimvuruge. Tumpe muda na nafasi ya kutuandalia mambo yetu.

Napenda kuhitimisha hotuba yangu kwa kumpongeza tena Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa uongozi wake unaotoa kipaumbele kwa ajenda ya maendeleo ya vijana. Dhamira yetu ni kujenga vijana wenye uwezo wa kuzalisha, kubuni na kumiliki shughuli za kiuchumi. Wizara, taasisi na kila mmoja wetu awajibike ili kufikia azma hiyo.

Mwisho, nawashukuru kwa kushiriki hafla hii muhimu kwa maendeleo ya vijana wa Taifa letu. Nawasihi nyote kuibeba ajenda hii kila mmoja mahali alipo ili kuwezesha vijana kushiriki kikamilifu katika kuijenga nchi yetu.

Ahsanteni kwa kunisikiliza.